**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/2025

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS (MBM)**
**WAZIRI WA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**

**MEI, 2024**

**YALIYOMO**


UTANGULIZI ..... 1

MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO ..... 5
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024 ..... 6
Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa ..... 6
Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji ..... 6
Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji ..... 8

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024. ..... 8
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ..... 10
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji ..... 10
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. ..... 11
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..... 12
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI ..... 12

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 13
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO ..... 14
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ..... 14
Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI ..... 15

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO ..... 16
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ..... 16
Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 16
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba ..... 17

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..... 18
Makadirio ya Mapato ..... 18
Makadirio ya Matumizi 2024/2025 ..... 18

MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. ..... 19
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ..... 19
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji ..... 19
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula ..... 20
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar ..... 20
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..... 21

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 22
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO ..... 22
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ..... 22

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO ....24
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ....24
Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ....24
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo – Pemba ...25

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ....25
SHUKURANI ....25

VIAMBATANISHO ....28
Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2022 -2023, Zanzibar ....28
Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2023 ....29
Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2023 ....30
Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2023 ....31
Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2023 ....32
Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2023 - Machi 2024 ....33
Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2023 Hadi Machi, 2024 ....34
Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 ....35
Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 ....36
Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji....38
Kiambatanisho Nam 7B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula 39
Kiambatanisho Nam. 7C: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) ....40
Kiambatanisho Nam. 7D: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R ....41
Kiambatanisho Nam. 7E: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT) ....42
Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kilimo Tija ....43
Kiambatanisho Nam. 7G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC) ....44
Kiambatanisho Nam. 7H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo ....45
Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha usalama wa chakula STREPHIT) ....46
Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR ....47
Kiambatanisho Nam. 7K: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji ....48
Kiambatanisho Nam. 7L: Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi ....49
Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2024/2025 ....50

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambapo inakadiriwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wake wanajihusisha na kazi za kilimo, ufugaji na uhifadhi wa maliasili.

3. **Mheshimiwa Spika,** pili napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, natoa pole kwa Rais wa Zanzibar pamoja na ndugu, jamaa na wananchi wote kwa ujumla kwa kuondokewa na kipenzi chetu Mstaafu Rais wa Jamhuri ya Muungano, Sheikh Ali Hassan Mwinyi, ambaye alifariki dunia siku ya tarehe 29 Februari 2024 na kuzikwa siku ya tarehe 2 Machi 2024. **Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi "Aamin"**

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuniamini kuingoza na kuisimamia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kipindi chote hiki. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumuhakikishia kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu na naahidi kwamba nitaitumikia Serikali hii kwa uwezo wangu wote kwa kutekeleza kwa vitendo ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 ili kuleta mageuzi katika sekta ya Kilimo nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa wakiwemo; Ndugu yangu mpenzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mhe. Shariff Ali Shariff, Waziri wa

Nchi Ofisi ya Rais- Ikulu Mhe. Ali Suleiman Ameir (Mrembo), Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mhe. Shaaban Ali Othman, na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuendeleza sekta ya kilimo. Aidha, ninawashukuru kwa maelekezo na miongozo yao wanayoitoa kwa sekta ya kilimo kwa kadri inavyohitajika.

7. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi kwa umakini na umahiri wako wa kuliendesha na kulisimamia Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaokusaidia kuliongoza Baraza hili na tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awazidishieni uwezo, hekima na busara ili mpate wepesi wa kuliendesha Baraza kwa ufanisi na mafanikio zaidi.

8. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Utalii, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Bumbwini pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushauri na miongozo wanayoitoa kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/2024. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, Mwakilishi wa Wananchi wa jimbo la Dimani, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2024/2025. Napenda kukuhakikishia kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupatia tumeyazingatia na kuyaweka katika bajeti hii ninayoiwasilisha.

9. **Mheshimiwa Spika,** mwisho na si kwa umuhimu napenda kuitumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Micheweni kwa kunipa mashirikiano na kuwa pamoja nami katika suala zima la kufanikisha maendeleo ya jimbo letu na ya nchi kwa ujumla. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta tija na maendeleo jimboni mwetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali katika kuendeleza

Sekta hii ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapunguza utegemezi wa mahitaji ya chakula; kwa kuendeleza kilimo biashara katika uzalishaji wa mazao ya chakula na kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Juhudi nyengine ni kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda pamoja na mazao ya mizizi ambayo ndiyo chachu ya maendeleo katika sekta ya viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la nazi na karafuu nchini. Vilevile, upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji wenye tija na matumizi ya mbegu bora za mifugo utaendelezwa. Wizara yangu pia itaendelea na usimamizi wa misitu ya hifadhi na ya jamii kwa lengo la kuhifadhi bioanuai, mazingira pamoja na kuimarisha huduma za utalii wa kimaumbile.

11. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inayojumuisha mazao, mifugo na maliasili za misitu bado ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha. Sekta ya Kilimo imeajiri takriban asilimia 35 ya wananchi wa Zanzibar na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii katika kujikimu kimaisha. Lengo kuu la Wizara ni kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza pato la Taifa sambamba na uhifadhi wa maliasili zetu. Kwa mwaka 2023 Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 24.9 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 25.9 iliyoripotiwa mwaka 2022.

12. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kwamba jumla ya eneo lililopandwa mazao mwaka 2023 limeongezeka hadi kufikia ekari 122,515 ikilinganishwa na ekari 104,316 za mwaka 2022, sawa na ongezeko la ekari 18,199. Kati ya eneo hilo, ekari 101,135 ambazo ni sawa na asilimia 82.55 zilipandwa mazao ya chakula. Zao la muhogo lilichukua eneo kubwa la ekari 37,549 ambazo ni sawa na asilimia 31 ya eneo lote lilopandwa mazao ya chakula kwa mwaka 2023, zao la mpunga lilipandwa katika eneo la ekari 29,519 ambazo ni sawa na asilimia 24, na mazao ya mboga na matunda yalipandwa katika eneo la ekari 21,380 ambazo ni sawa na asilimia 17 **(Kiambatanisho Nam. 1)**. Hivyo, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kulima mazao ya chakula, mboga, matunda na viungo ili kutosheleza soko la ndani likiwemo la utalii sambamba na kuongeza pato la Taifa.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kwa tofauti ya tani 186,904 kutoka tani 342,181 mwaka 2022 ikilinganishwa na tani 529,085 mwaka 2023. Ongezeko hili la uzalishaji limetokana na kushajiika kwa wakulima kuongeza juhudi katika kilimo ikiwa ni

pamoja na kupanda mazao yanayohimili ukame ikiwemo muhogo, viazi vitamu na maboga. Uzalishaji wa zao la muhogo umeongezeka kutoka tani 202,519 za mwaka 2022 hadi kufikia tani 220,412 mwaka 2023 na Viazi vitamu vimeongezeka kutoka tani 40,286 za mwaka 2022 hadi kufikia tani 53,914 mwaka 2023. Kwa upande wa zao la mpunga, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 27,947 mwaka 2022 hadi tani 37,272 mwaka 2023 kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ambayo tayari imeanza uzalishaji. Aidha, uzalishaji wa mboga na matunda umeongezeka kwa tofauti ya tani 21,667 kutoka tani 66,304 mwaka 2022 hadi kufikia tani 87,971 mwaka 2023, kutokana na wananchi wengi kuhamasika na kilimo cha umwagiliaji kwenye matunda na mboga.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, uzalishaji umepungua kutoka tani 4,734.1 mwaka 2022 hadi tani 2,654.7 za mwaka 2023 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 43.9. Hali hii imetokana na kuwa na msimu mdogo wa uzalishaji. Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa zao hili kwa kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora, elimu ya uoteshaji na uhuishaji.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa uchinjaji wa ng'ombe kutoka 27,326 mwaka 2022 hadi 29,851 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 9.2. Aidha, idadi ya mbuzi na kondoo waliochinjwa imeongezeka kutoka 4,465 mwaka 2022 hadi mbuzi na kondoo 13,977 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 213. **(Kiambatanisho Nam. 2A)**. Idadi ya kuku waliochinjwa imeongezeka hadi kufikia kuku 1,161,238 mwaka 2023 ukilinganishwa na kuku 1,130,981 mwaka 2022 **(Kiambatanisho Nam. 2B)**. Aidha, uchinjaji wa wanyama wengine umeripotiwa kwa ongezeko la bata 2,865 mwaka 2023 kutoka bata 2,150 mwaka 2022, simbilisi 418 na sungura 343 **(Kiambatanisho Nam. 2C)**.

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mazao ya misitu, takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2023 matumizi ya kuni yamepungua kutoka mita za ujazo 26,236 mwaka 2022 hadi mita za ujazo 25,909.7 mwaka 2023. Matumizi ya boriti (majengo) yameongezeka kutoka mita za ujazo 1,741 mwaka 2022 hadi 2053.5 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 18. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kuezekea umepungua kutoka mita za ujazo 2,970 mwaka 2022 hadi mita za ujazo 2,264 mwaka 2023. Uzalishaji wa nguzo kubwa umepungua kutoka mita za ujazo 2,948 mwaka 2022 hadi mita za ujazo 2,084.8 mwaka 2023 **(Kiambatanisho Nam. 3)**. Matumizi ya kuni kwa upande wa wananchi, hasa wa mijini, yamepungua kutokana kuhamasika katika matumizi ya nishati mbadala ya kupikia ikiwemo gesi na umeme. Wizara inaendelea kuhamasisha

jamii kutumia mbinu mbadala kwa nishati na ujenzi ili kunusuru misitu na bioanuai zilizomo.

## MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO

**17. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imeundwa na Idara sita (6) ambazo ni Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, Idara ya Umwagiliaji Maji, Idara ya Misitu, Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Aidha, zipo Taasisi tatu (3) ambazo ni Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo; pamoja na Ofisi Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Wizara - Pemba. Wizara ina jumla ya wafanyakazi wa kudumu 2,383 (Unguja 1,848 na Pemba 535) wakiwemo wanaume 1,234 na wanawake 1,149.

**18. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina majukumu makuu yafuatayo:

1. Kusimamia maendeleo ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara, huduma za pembejeo na zana za kilimo, huduma za ugani (elimu kwa wakulima) pamoja na uhifadhi na ukaguzi wa mazao;
2. Kulinda, kuhifadhi na kusimamia rasilimali za misitu na wanyamapori;
3. Kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa sekta za kilimo (mazao, mifugo na misitu) na kutoa matokeo yake kwa wadau;
4. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti pamoja na kuratibu mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi wakiwemo washirika wa maendeleo na sekta binafsi; na
5. Kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala ikiwa ni pamoja na masuala ya mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu pamoja na uratibu wa masuala mtambuka ikiwemo ukimwi na jinsia.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024

### Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa

19. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/24, ilikadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni **5.53** kupitia vianzio vyake kumi na moja (11) vilivyopo Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Wizara imeweza kukusanya TZS bilioni **2.964** sawa na asilimia **70** ya lengo la makisio kwa robo tatu ambalo ni sawa na asilimia **53.56** ya makadirio ya mwaka (**Kiambatanisho Nam 4).**

### Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/24 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

a. Kufanyia mapitia Sera ya Kilimo ya mwaka 2002 pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo, nyaraka ambazo zipo katika taratibu za mwisho za Serikali kabla ya kuidhinishwa;

b. Kukamilika kwa miundombinu mipya ya Umwagiliaji katika mabonde ya Cheju A', Kinyasini, Kibokwa, Kilombero, Chaani na Mlemele yenye jumla ya hekta 1,053 na hivyo kufikisha jumla ya hekta 1,928 za umwagiliaji kutoka hekta 875 za miundombinu ya zamani. Miundombinu hii imeongeza tija katika uzalishaji wa mpunga na kufikia uzalishaji wa wastani wa tani 5.5 kwa hekta kwa msimu na tani 11 kwa hekta kwa mwaka;

c. Kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa mpunga kufikia ekari 29,520 (Unguja ni 11,018 na Pemba ni 18,502) ambapo kumechochea ongezeko la mavuno kufikia tani 37,272;

d. Kuchunguza afya ya udongo na kutoa matokeo yake bila ya malipo kwa wakulima 500 (Unguja 300 na Pemba 200);

e. Jumla ya miche 1,695,553 ikiwemo ya mikarafuu (134,777), minazi (49,050), misitu (590,336) na matunda na viungo (921,390) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali na watu binafsi;

f. Wizara imefanikiwa kupandisha hadhi Msitu wa 'Kidikotundu-Nongwe-Vundwe', uliopo mkoa wa Kusini Unguja, kutoka hifadhi ya jamii na kuwa hifadhi ya msitu wa Serikali ambapo hadhi hiyo italeta chachu ya utalii wa Kimaumbile na Uhifadhi wa bioanuai;

g. Jumla ya watalii 55,870 walitembelea Hifadhi wakiwemo (44,805 kutoka nje na 11,065 wa ndani). Aidha, TZS 1,064,580,200 na Dola za kimarekani 43,419 zilikusanywa ikiwa ada za viingilio;

h. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama, jumla ya Kuku 71,840 (63,974 Unguja na 7,866 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya tofauti, Mbwa 6,191 (5,151 Unguja na 1,040 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies) na Ng'ombe 1,506 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (Black Quarter) na kimeta (Anthrax).

21. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara yangu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a. Matukio ya mifumo ya kuhalalisha wizi wa mazao, ambapo baadhi ya madalali hununua bidhaa za wizi na kuzifikisha sokoni bila kufahamika;

b. Upungufu wa wataalamu wa kada za kilimo, mifugo na maliasili unaotokana na wimbi kubwa la wataalamu kustaafu au kuhamishiwa sekta nyengine wakiwemo mabibi na mabwana shamba;

c. Uvamizi wa maeneo ya kilimo unaosababishwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa makaazi na shughuli nyengine za kimaendeleo;

d. Uwepo wa bei kubwa ya pembejeo za kilimo;

e. Kuendelea kwa athari ya mabadiliko ya tabianchi kunakopelekea uhaba wa mvua, maradhi katika mazao na upungufu wa malisho kwa mifugo;

f. Kuendelea kwa uharibifu wa misitu unaotokana na shughuli za kibinadamu kama vile uvunaji wa asali kwa kutumia njia za kienyeji; na

g. Upungufu wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri, ofisi za Wilaya na vifaa vya ofisi.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

a. Kuangalia upya taratibu za udhibiti wa mazao na mifugo mashambani kabla ya kuyasafirisha kuelekea sokoni. Tunaomba vyombo husika viendeleze jitihada za kutatua changamoto ya wizi wa mazo na mifugo;

b. Kuwasilisha mapendekezo ya uajiri Ofisi Kuu ya Utumishi Serikalini;

c. Kukamilisha Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo ambapo utekelezaji wake unategemewa kutatua changamoto nyingi za kiutendaji zilizoainishwa;

d. Kuendelea na utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima; na

e. Kufanya tafiti juu ya mazao ya kilimo na mifugo yanayohimili athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhamasisha wananchi kulima na kufuga.

**Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji**

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, iliidhinishiwa kutumia TZS bilioni 98.716, kati ya fedha hizo TZS bilioni 20.461 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 16.887 kwa Mishahara na TZS bilioni 3.574 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 9.731 ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni 8.301 kwa Mishahara na TZS bilioni 1.430 kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara iliombewa TZS bilioni 68.524 (TZS bilioni 43.524 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni 25.000 kutoka SMZ).

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 Wizara imepata TZS bilioni 47.694 sawa na asilimia 48.31 ya fedha zilizoidhinishwa, kati ya hizo TZS bilioni 12.686 zimetumika kwa matumizi ya kawaida (TZS bilioni 11.557 kwa mishahara na TZS bilioni 1.129 kwa matumizi mengineyo). Aidha, ruzuku ya Serikali kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta ni TZS bilioni 6.446 (TZS bilioni 5.809 kwa mishahara na TZS milioni 637.067 kwa matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imepata TZS bilioni 28.561 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **(Kiambatanisho Nam. 5).**

**UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024.**

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya

Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 - 2026 na Mipango Mkakati ya Kisekta ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Utekelezaji wa Mikakati hii umesaidia kuongeza uzalishaji na tija hususan kwa mazao ya mboga na matunda.

**27. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutekeleza shabaha zake kupitia programu kuu nne na Miradi minane ya Maendeleo. Programu hizo ni kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

Aidha, Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

i. Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji;
ii. Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa chakula;
iii. Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC);
iv. Mradi wa Kudhibiti Nzi Waharibifu wa Matunda;
v. Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (Agriconnect);
vi. Mradi wa Kilimo Tija;
vii. Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC); na
viii. Mradi wa kuendeleza Miundombinu ya Mifugo.

**28. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ilikusudia kutekeleza shabaha ziuatazo:

1. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

2. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo utoaji wa elimu, udhibiti wa magonjwa na uwepo wa uhakika wa chakula;

3. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

4. Kuendeleza na kuimarisha tafiti za kilimo, maliasili na mifugo;

5. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 2,000,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;

6. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;

7. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na

8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO**

**29. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo nne zifuatazo:

i. Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;
ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula;
iii. Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo; na
iv. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji**

**30. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Ujenzi wa misingi ya kumwagilia maji kwa kiwango cha saruji (lining of tertiary canals) yenye jumla ya urefu wa kilomita 35.3 katika mabonde ya; Chaani, Kibokwa, Cheju A, Kilombero na Mlemele umekamilika;

b. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la Cheju B' sambamba na kazi za uchimbaji wa misingi mikubwa na midogo ya kutolea maji ya ziada unaendelea;

c. Ujenzi wa uzio (fence) katika bwawa la Kinyasini (mita 400) na Chaani (mita 1300) umekamilika;

d. Kazi za kutoa na kuweka pampu na vifaa vya umeme (Breaker na Phase Failure Relay) katika visima vya Cheju, Mtwango na Bumbwisudi zimeendelea. Aidha, kazi za kufanya tathmini na ukarabati wa vibanda vya pampu katika visima vya Cheju na Kibokwa zimefanyika; na

e. Jumla ya mikutano 136 (71 ya wakulima viongozi na 65 ya wakulima wa kawaida) ya kupanga na kujadili maendeleo ya kilimo cha mpunga katika mabonde yote ya Umwagiliajimaji; pamoja na kazi ya kutoa mafunzo kwa wakulima 500 (wanaume 218 na wanawake 282) kati ya hao wakiwemo vijana 78 na watu wazima 422 zimefanyika. Aidha, fidia kwa wananchi 31 walioathirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi

wa miundombinu katika mabonde ya Chaani, Kilombero na Mlemele imelipwa.

**31. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 33.584 ambapo TZS bilioni 1.883 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 1.470 Mshahara na TZS milioni 412.800 kwa matumizi mengineyo). Vilevile, programu iliombewa TZS bilioni 31.701 kwa kazi za maendeleo ambapo TZS bilioni 31.701 kutoka kwa wahisani EXIM BANK ya Korea na TZS milioni 500.000 kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imepata TZS bilioni 22.355. Kati ya fedha hizo TZS milioni 971.133 kwa Mishahara, TZS milioni 83.451 kwa matumizi mengineyo na TZS bilioni 21.300 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.**

**32. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya ekari mbili (2) zimepandwa mbegu ya mpunga katika bonde la Mwera na Kibonde mzungu. Aidha, jumla ya kilogramu 840 za mbegu mama zimezalishwa;

b. Kwa kushirikiana na ofisi ya E-government Wizara imeendelea kuweka mahitaji ya msingi ya kuandaa Mfumo wa Kidijitali wa kutambua mahitaji ya pembejeo kwa wakulima wa mpunga;

c. Jumla ya miche 134,777 ya mikarafuu na miche 49,050 ya minazi imeoteshwa katika vitalu vya Serikali. Aidha, miche 353,540 ya miti ya matunda na viungo imeoteshwa katika vitalu vya Serikali (53,540) na vya watu binafsi (300,000);

d. Mkataba wa mashirikiano (MOU) baina ya Wakala wa Akiba ya Chakula (National Food Reserve Agency) – Tanzania bara na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa ajili ya ununuzi wa akiba ya chakula tayari umesainiwa;

e. Taratibu za manunuzi za kumpata mjenzi wa maghala na vihenge (Silos) kwenye eneo la Bungi Unguja na Chamanagwe Pemba umefikia katika hatua za mwishoni. Aidha, ukarabati wa maghala mawili ya kuhifadhia chakula yaliyopo Malindi Unguja umekamilika.

**33. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 39.223 ambapo TZS bilioni 4.912 kwa kazi za kawaida

(TZS bilioni 4.012 kwa Mshahara na TZS milioni 900.100 kwa matumizi mengineyo) TZS bilioni 34.311 kutoka kwa Miradi ya Maendeleo, TZS bilioni 25.500 kutoka SMZ na TZS bilioni 8.811 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imepata TZS bilioni 9.847 (TZS bilioni 2.717 ni Mishahara na TZS milioni 133.458 kwa matumizi mengineyo), kwa fedha za Maendeleo zilizopatikana ni TZS bilioni 6.997 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

34. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya ekari 4,016.5 kwa ajili ya kilimo cha mpunga zimelimwa (Unguja 2,519.5 na Pemba 1,497). Aidha, Wakala imeendelea na ununuzi wa vipuri vya matrekta na vilainishi (lubricant) ambapo jumla ya matrekta 27 (Unguja 20 na Pemba 7) yamefanyiwa matengenezo madogo na tayari yanaendelea kutoa huduma za ukulima; na

b. Kazi ya uhamasishaji jumuiya za wakulima kulima kwa wakati ili kupunguza uhitaji wa matrekta kwa wakati mmoja inaendelea.

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 2.383 (TZS bilioni 1.702 kwa Mshahara na TZS milioni 680.100 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imepata TZS bilioni 1.062 ambapo (TZS milioni 595.314 kwa ajili ya Mishahara na TZS milioni 464.765 kwa matumizi mengineyo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI**

36. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Uvunaji wa jaribio la muhogo ambapo jumla ya aina kumi (10) za mbegu zimechaguliwa kati ya hizo aina nane (8) ni mpya, aina moja iliyoboreshwa (improved) na aina moja ya kienyeji. Aina hizi za mbegu zilichaguliwa kwa kigezo cha uwezo wa kustahamili mradhi ya michirizi kahawia ("Cassava Brown Streak Desease") na Bato Bato, pia aina hizo za mbegu zimetoa mavuno mazuri;

b. Jumla ya aina 66 za mbegu za mpunga kutoka IRRI zilipandwa katika bonde la Kinyasini kwa ajili ya kuzitafiti ubora wake katika ukuaji na uzazi. Jaribio hili limevunwa na kuanza kufanyiwa uchambuzi wa kitaalamu kwa

kutumia takwimu zilizokusanywa ili kugundua aina bora za mbegu kati ya hizo 66;

c. Aina 15 za mbegu za kienyeji za mpunga zilipandwa ili kuendeleza kizazi cha mbegu hizo kisipotee kwa ajili ya matumizi ya baadae. Mbegu hizo tayari zimeshavunwa na kuhifadhiwa. Aidha, jaribio la njugu nyasa limekamilika na aina kumi (10) kati ya 35 zimechaguliwa kuendelea na uchunguzi mashambani badala ya kituoni;

d. Utafiti wa matumizi ya mwani kuwa mbolea ya migomba unaendelea;

e. Andiko la kisayansi la matokeo ya jaribio la viatilifu asili katika kumdhibiti nzige wa kabichi ya Kichina (Diamond Back Moth) limechapishwa katika Jarida la "Acta agriculturae Slovenica" 119/4, 1-6, Ljubljana 2023;

f. Utafiti wa afya ya udongo na uimarishaji wa mnyororo wa thamani Zanzibar unaendelea; ambapo wakulima 198 (Unguja 94, Pemba 104) walipata mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora za mbogamboga ("Quality Declared Seeds"), sampuli za udongo 150 zilikusanywa kwa kufanyiwa uchunguzi nje ya nchi kwa lengo la kutengeneza ramani ya udongo ya Zanzibar na sampuli 500 za udongo kutoka kwa mkulima mmoja mmoja ndani ya wilaya kumi za Zanzibar (50/wilaya) zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa virutubisho;

g. Ujenzi wa "Screen house" maalum kwa zao la mpunga hapo Kizimbani Unguja umekamilika.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 5.353 (TZS bilioni 4.953 kwa Mshahara na TZS milioni 400.000 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imepata TZS bilioni 3.909 (TZS bilioni 3.842 kwa Mishahara na TZS milioni 66.552 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia ya fedha iliyoidhinishwa.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**38. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii katika Programu Ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya miche 358,929 (316,686 Unguja na 42,243 Pemba) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali na Miche 841,500 (542,600 Unguja na 298,900 Pemba) imeoteshwa katika vitalu vya watu binafsi;

b. Jumla ya Hekta 29.5 zilipandwa miti kwa kushirikiana na jamii kati ya hizo hekta 5 zimepandwa miti ya mikoko;

c. Jumla ya watalii 55,870 walitembelea Hifadhi na kuingiza mapato ya jumla ya TZS bilioni 1.065 pamoja na Dola za kimarekani 43,419;

d. Kupandisha hadhi Msitu wa Kidikotundu-Nongwe-Vundwe ambapo hatua zinazoendelea ni kuandaa Mpango wa Usimamizi wa hifadhi hiyo;

e. Jumla ya doria 522 zilifanyika (325 Unguja na 197 Pemba) ambapo matukio 138 (105 Unguja na 33 Pemba) yaliripotiwa yakiwemo usafirishaji wa mazao ya misitu bila ya vibali, matumizi mabaya ya msumeno wa moto, uharibifu wa misitu, uchimbaji wa mchanga na mawe, upikaji wa pombe za kienyeji, uchomaji moto pamoja na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa kilimo na ujenzi wa nyumba za Makaazi.

**39. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa TZS bilioni 3.457 (TZS bilioni 2. 512 mishahara na TZS milioni 430. 500 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imepata TZS bilioni 1.983 ambapo TZS bilioni 1.641 kwa mishahara, TZS milioni 77.206 kwa matumizi mengineyo na TZS milioni 264.000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO**

**40. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina Programu Ndogo mbili za Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo, pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI).

**Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo**

**41. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo kwa Mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Ng’ombe 1,467 (749 Unguja na 718 Pemba) wamepandishwa kwa njia ya sindano;

b. Ekari nane (8) za malisho aina ya JUNCAO yamepandwa kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za malisho;

c. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama kuku 71,840 (63,974 Unguja na 7,866 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya kuku tofauti, mbwa 6,191 (5,151 Unguja na 1,040 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa

wa kichaa cha mbwa (Rabies) na ng'ombe 1,506 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (Black Quarter) na kimeta (Anthrax);

d. Sampuli 511 (379 Unguja na 132 Pemba) zilichunguzwa maradhi mbalimbali katika maabara na sampuli 328 zilizoonekana na vimelea vya maradhi kama vile ya kuharisha damu (Coccidiosis) kwa kuku, kichaa cha mbwa (Rabies) kwa mbwa na paka, ndigana kali (East Coast Fever), ugonjwa wa kiwele (Mastitis) kwa ng'ombe, minyoo kwa kuku, ng'ombe na mbuzi na usugu wa vimelea vya maradhi dhidi ya madawa kwa kuku. Sampuli hizo zimechunguzwa kwenye kinyesi, ubongo, damu na maziwa;

**42. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 5.304 ambapo TZS bilioni 3.304 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 2.752 kwa mishahara na TZS milioni 552.000 kwa matumizi mengineyo). Vilevile, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 2.000 kwa ajili ya Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo. Hadi kufikia Machi, 2024 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 1.971, ambapo TZS bilioni 1.877 kwa mishahara na TZS milioni 94.350 kwa matumizi mengineyo.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI**

**43. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Tathmini ya ufanisi wa malisho (Brachiaria) imekamilika, Utafiti wa mbuzi wa kienyeji pamoja na machotara wao unaendelea;

b. Utafiti wa Mbuzi wa Zanzibar kwa ukusanyaji wa Minyoo umeanza kwa Wilaya za Kusini, Kaskazini B', Kati na Magharibi A' kwa Unguja. Utafiti huu umejumuisha wafugaji wa nane (8) kwa kila Shehia ambapo wastani wa mbuzi 3 – 5 wamechukuliwa sampuli ya minyoo;

c. Jumla ya ekari saba (2 Unguja na 5 Pemba) za majani ya malisho zimeoteshwa); na

d. Ujenzi wa mnara kwa ajili ya kurahisisha umwagiliaji wa malisho umefanyika Chamanangwe Pemba na kazi ya umwagiliaji inaendelea;

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya TZS bilioni 1.996 (TZS bilionio 1.646 kwa mishahara na TZS milioni 350.300 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 1.476 (TZS bilioni 1.370 kwa mishahara na TZS milioni 105.750 kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO**

**45. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo;
ii. Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; na
iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo – Pemba.

**Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo**

**46. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Wafanyakazi 42 wamepatiwa stahiki zao ikiwemo ubani (6) likizo (28) na muda wa ziada (8) ambapo jumla ya TZS 9,830,000/= zimetumika;

b. Jumla ya wafanyakazi watano (5) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; na

c. Wizara imewasilisha orodha ya maeneo ya ardhi yanayohitaji kusajiliwa kwa Wizara ya Ardhi.

**47. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS bilioni 2.441 (TZS bilioni 1.733 kwa mshahara na TZS milioni 707.558 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 1.447 (TZS bilioni 1.099 kwa mishahara na TZS milioni 347.958 kwa matumizi mengineyo).

**Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

**48. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Mapitio ya Sera ya kilimo ya mwaka 2002 yamekamilika na sasa yamewasilishwa katika kamati ya Makatibu Wakuu kwa mapitio na baadae kupelekwa kikao cha Baraza la Mapinduzi. Aidha, Mapitio ya Sera ya Misitu ya mwaka 1995, Mapitio ya Sheria ya Udhibiti wa mimea yanaendelea kwa hatua za uwandishi wa Waraka kupelekwa kwa Makatibu Wakuu na Mpango wa Mageuzi ya sekta ya Kilimo umepitiwa na kuwasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba na sasa upo katika hatua za kujumuisha maoni

hayo na baadae kupelekwa kwenye Kamati Tendaji ya Wizara na Kamati ya Uongozi;

b. Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inatekeleza Mradi wa 50x2030 wenye lengo la kuimarisha Takwimu za Kilimo na kuweka viwango vinavoendana na Duniani. Programu hii ina lengo la kuchangia ongezeko la uhakika wa chakula na lishe, kupunguza njaa na kilimo endelevu ambapo tayari imeshakusanya taarifa kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba na kinachoendelea ni uhakiki wa takwimu hizo.

c. Wizara imeshiriki katika ziara za nchini Italia ambapo ilifadhiliwa na shirika la chakula FAO lengo la mkutano huo ni muendelezo wa mikakati ya Tanzania kuimarisha mifumo ya chakula nchini na sasa Wizara imeshaandaa MoU ya miradi hiyo na kufanya mazungumzo na Ubalozi wa Italia nchini Tanzania. Aidha Wizara imeshiriki katika mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika nchini Dubai;

d. Wizara kwa kushirikiana na TAHA imefanya ziara ya pamoja katika Mkoa wa Arusha ambapo imewashirikisha wajumbe wa kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa lengo la kujifunza shughuli za kilimo katika Mkoa huo; na

e. Utafiti mmoja wa kuangalia mazao ya kilimo yanayopelekwa katika masoko ya utalii ulifanyika kwa lengo la kuangalia fursa na changamoto zilizopo. Utafiti umegundua kwamba asilimia 11 ya wakulima wanauza mazao yao katika masoko ya utalii. Miongoni mwao asilimia 35 wanauza zao moja tu, asilimia 5 wanauza mazao mawili na asilimia 60 wanauza zaidi ya mazao mawili.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS milioni 563.139 kwa kazi za kawaida (TZS milioni 318.889 Mishahara na TZS milioni 244.250 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu Ndogo hii imepata TZS milioni 297.905 (TZS milioni 234.949 kwa mishahara na TZS milioni 62.956 kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba**

50. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

a. Ziara za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba ziliratibiwa;

b. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

c. Kuratibu ziara za wageni na viongozi pamoja na kuhudhuria katika vikao, sherehe na kumbukumbu za kitaifa; na

d. Changamoto za wadau zilitatuliwa pamoja na kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine (za Serikali, Sekta binafsi, na Taasisi za Kijamii).

**51. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 4.415 (TZS bilioni 4.088 kwa mishahara na TZS milioni 326.792 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2024 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 3.347 (TZS bilioni 3.017 kwa mishahara na TZS milioni 330.000 kwa matumizi mengineyo).

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Makadirio ya Mapato

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imekadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni **5.704** kupitia vianzio vyake 11 viliopo Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 6A).**

### Makadirio ya Matumizi 2024/2025

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, inaomba kuidhinishiwa kutumia **TZS bilioni 128.108** kupitia Programu zake kuu nne, kati ya fedha hizo TZS bilioni 23.423 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 19.134 ni Mishahara na TZS bilioni 4.289 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 11.197 ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni 9.520 Mishahara na TZS bilioni 1.677 kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

**54. Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya TZS bilioni **93.489** (TZS bilioni **63.489** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni **30.000** kutoka SMZ) (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

**MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.**

**55. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

1. Kuendelea Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;
2. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo ujenzi wa vituo vya huduma za kilimo mawilayani.
3. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwemo ndizi na mpunga, mboga na matunda na uzalishaji wa asali kwa kufanya tafiti, utaalamu na kusambaza teknologia kwa wakulima.
4. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;
5. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 1,700,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;
6. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;
7. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na
8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO**

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji**

**56. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji itatekeleza shabaha zifuatazo:

1. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagliaji yenye ukubwa wa eneo la hekta 131 katika bonde la Cheju B sambamba na kazi za ujenzi wa mitaro midogo yenye urefu wa Kilomita 20 kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Kilombero, Cheju na Kinyasini;

2. Kuimarisha na kukarabati miundombinu, huduma za usafiri, umeme, mawasiliano (mtandao), safari za kikazi na maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa.

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo hii inaombewa kuidhinishiwa TZS bilioni 27.698 kati ya hizo TZS bilioni 2.198 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 1.658 Mishahara na TZS milioni 540.000 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 25.500 kwa ajili ya Miradi kutoka washirika wa maendeleo.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula**

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika Chakula itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo ikiwemo elimu kwa wakulima na udhibiti wa magonjwa ya mimea;
2. Kuwatembelea wakulima na kuwapatia ushauri wa kitaalamu na kusambaza teknolojia mpya;
3. Kuotesha miche 700,000 (400,000 Mikarafuu na 300,000 Miti ya matunda na viungo) na kuigawa bure kwa wakulima;
4. Kuimarisha uwepo wa uhakika wa chakula;
5. Uzalishaji mbegu za mpunga;
6. Uimarishaji wa afya ya mimea nchini.

**59. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS bilioni 62.591 kati ya hizo TZS bilioni 5.785 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 4.713 kwa Mishahara na TZS bilioni 1.072 kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu inaombewa TZS bilioni 56.806 kwa miradi ya maendeleo (TZS billion 27.500 kutoka SMZ na TZS bilioni 29.306 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar**

**60. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu Ndogo hii inajumuisha shughuli za Utafiti wa Kilimo na Mifugo ambazo zimeunganisha Taasisi mbili za Utafiti wa Kilimo na Utafiti wa Mifugo, na itatekeleza shabaha zifuatazo:

1. Kuendelea na tafiti 4 zilizopo na kufanya tafiti mpya sita (6) za kilimo na maliasili; pamoja na tafiti 6 za mifugo ikiwemo tafiti za minyoo ya mbuzi na utafiti wa majani ya malisho ya mifugo na kuendeleza mashamba ya malisho ekari 10 (Chamanangwe 6 na Kizimbani 4).

2. Kufanya tafiti 11 mpya ikiwemo, utafiti wa kuangalia ufanisi wa majani ya malisho ya JUNCAO na matumizi ya mbegu za fenesi katika chakula cha kuku wa nyama na Utafiti wa matumizi ya mbegu za papai katika kudhibiti minyoo ya sungura;

3. Kuimarisha miundombinu ya utafiti ikiwemo kujenga na kukarabati baadhi ya majengo;

4. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kufanya mafunzo ya muda mrefu au mfupi; na

5. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwemo ununuzi wa vifaa na huduma za kiofisi.

**61. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 9.035, kati ya hizo (TZS bilioni 7.835 Mishahara na TZS bilioni 1.200 kwa matumizi mengineyo).

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

**62. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo itatekeleza shabaha zake kama zifuatazo:

1. Kuendeleza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za Kilimo, pamoja na kuhakikisha kuwepo vifaa vya kazi, vipuri na vilainishi; na

2. Kuhamasisha sekta binafsi katika kuekeza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za kilimo.

**63. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya jumla ya TZS bilioni 2.161 kati ya hizo (TZS bilioni 1.685 Mishahara na TZS millioni 476.100 kwa matumizi mengineyo).

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi wanaotembelea hifadhi kutoka 64,000 hadi kufikia 100,000 kwa kuimarisha vivutio na kuhamasisha miradi ya uwekezaji katika maeneo ya hifadhi za Misitu kwa lengo la kuongeza mapato;
2. Kukamilisha taratibu za upandishaji hadhi Msitu wa Mtambwe, na kukamilisha kufanya tafiti ya miradi ya kuinua kipato cha wanajamii wanaoishi karibu na Misitu huo;
3. Kuotesha miche 1,000,000 (800,000 Misitu na 200,000 Matunda na Viungo) na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahudumu 165;
4. Kuhamasisha na kupanda miti hekta 130 (Hekta 100 misitu ya Serikali, na Hekta 30 maeneo ya Mikoko) pamoja na kufanya tathmini ya hali ya miti iliyohuika;
5. Kuendeleza na kutoa elimu kwa jamii na kuimarisha ulinzi kwa kufanya doria 500 katika maeneo ya Misitu ya Hifadhi na Misitu ya Jamii Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza matukio ya uharibifu;
6. Kuengeza uzalishaji wa asali na mazao mengine ya nyuki kutoka tani 13 kufikia tani 17 kwa kutoa elimu bora ya ufugaji, utunzaji wa kumbukumbu na kuhamasisha kwa ugawaji wa vifaa vya kufugia nyuki; na
7. Kufanya tafiti ya kubaini idadi aina na hali ya wanyamapori kwa lengo la kuandaa mpango wa kunusuru wanyama waliohatarini kutoweka pamoja na kusimamia mazizi.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 4.504 kati ya hizo (TZS bilioni 2.791 Mishahara, TZS millioni 530.00 kwa matumizi mengineyo na TZS bilioni 1.183 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

### Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kupandisha Ng’ombe 2,000 (1,200 Unguja na 800 Pemba) kwa njia ya sindano;

2. Kupanda eka 10 za malisho katika shamba la malisho Kizimbani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za majani ya malisho ya mifugo na kuwapatia wafugaji 1,000 (600 Unguja na 400 Pemba) ili waoteshe katika mashamba yao kwa ajili ya kulisha mifugo;

3. Kutoa mafunzo 20 (12 Unguja na 8 Pemba) ya mbinu bora za ufugaji wa ng’ombe, mbuzi na kuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao;

4. Kuwatembelea wafugaji 17,000 (Unguja 9,000 na Pemba 8,000) na kuwapa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji;

5. Kuchanja kuku 250,000 (180,000 Unguja na 70,000 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa mahepe, gumboro na ndui, mbwa 8,000 (Unguja 5,000 na Pemba 3,000) dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies) na ng’ombe 35,000 (23,000 Unguja na 12,000) dhidi ya magonjwa chambavu (Black Quanter), kimeta (Anthrax), ugonjwa wa ngozi (Lumpy Skin Disease) na ugonjwa wa miguu na midomo (Foot and Mouth Disease);

6. Kufunga uzazi mbwa 50 na paka 350 ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji;

7. Kuchunguza sampuli 1,500 (1,000 Unguja na 500 Pemba) za maradhi ya mifugo; na

8. Uanzishaji wa mfumo wa kielectroniki wa ufutiliaji wa magonjwa ya mifugo.

**67. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 13.890 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo (TZS bilioni 3.230 kwa Mishahara na TZS millioni 660.500 kwa matumizi mengineyo). Aidha, inaombewa TZS bilioni 10.000 kwa miradi ya maendeleo (TZS bilioni 2.500 kutoka SMZ na TZS bilioni 7.500 kutoka kwa washirika wa maendeleo).

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

### Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 100, ikiwemo ubani (20), likizo (50), na muda wa ziada (30);
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 58 kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi pamoja na wanafunzi (madaktari wa mifugo 23);
3. Kuwapatia mafunzo ya kujiandaa na kustaafu wafanyakazi 50;
4. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali TZS bilioni 5.704; na
5. Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali.

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 2.578 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 1.829 kwa Mishahara na TZS millioni 749.000 kwa matumizi mengineyo).

### Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

**70. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi iliyopo chini ya Wizara;
2. Kuimarisha ukusanyaji wa Takwimu za kisekta;
3. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa; na
4. Kufanya tafiti mbili za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti wa Zanzibar.

**71. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti inaomba kuidhinishiwa TZS milioni 747.790 kwa kazi

za kawaida (TZS milioni 411.690 Mishahara na TZS milioni 336.100 kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo – Pemba**

**72. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba itatekeleza shabaha yake kuu kama ifuatavyo:

Kuratibu na kusimamia kazi za kilimo, umwagiliaji, maliasili na mifugo Pemba.

**73. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za kilimo umwagiliaji maliasili na mifugo Pemba inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 4.901 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 4.500 Mishahara na TZS millioni 401.000 kwa matumizi mengineyo).

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**74. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS bilioni **5.704** kupitia vyanzo vyake Unguja na Pemba.

**75. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, inaomba kuidhinishiwa kutumia TZS bilioni 128.108, kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo zikijumuisha ruzuku ya TZS bilioni 11.197 kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo pamoja na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza miradi kumi na mbili kama inavyoonekana kwenye **Kiambatanisho Nam. 7A – 7L.** Utekelezaji wa Miradi hiyo inaombewa TZS bilioni 93.489 (TZS bilioni 30.00 kutoka SMZ na TZS bilioni 63.489 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Aidha, Wizara itatelekeza Programu Kuu nne kama zinavyoonekana katika **Kiambatanisho Nam 8.**

**SHUKURANI**

**77. Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili na mifugo; zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Ofisi ya Rais - Fedha na

Mipango, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Ofisi ya Rais - Kazi Uchumi na Uwekezaji, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

78. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za pekee ziende kwenye Wizara na Taasisi zinazoshabihiana na Wizara ya Kilimo kwa upande wa Tanzania Bara. Wizara na Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kamisheni ya Umwagiliaji Maji, Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA), CARI, NFRA Uongozi wa Mikoa ya Morogoro, Tanga, Arusha na Kilimanjaro.

79. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru Mashirika binafsi ya ndani na nje ya nchi yakiwemo PBZ, CRDB, EQUITY BANK, ADB, ZSTC, PDF, TAHA, UWAMWIMA, FEED THE FUTURE, COSTECH, COMMUNITY FOREST PEMBA, ENABEL, TAFIRI, TALIRI, TPHPA, TPRI, ZAASO na ZSPCA. Tunazishukuru pia nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia kuendeleza sekta hii, zikiwemo Japan, China, Korea ya Kusini, Marekani, UAE, Oman, Italia na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo. Benki ya Dunia, Benki ya Tanzania ya Kilimo, Benki ya Umoja wa nchi za Ulaya - EU, Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), ICRAF, IFAD, UNDP, JICA, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, WCS, GARC, PASS, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Root and Shoot, Solidaridad, NMB, Heifer International, Exim Bank ya Korea, FLI ya Ujerumani na World Vegetable Centre.

80. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara hii ninayoiongoza wakiwemo; Katibu Mkuu – Ndugu Ali Khamis Juma, Naibu Katibu Mkuu – Dk. Omar Ali Amir, Ofisa Mdhamini WKUMM, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara na Bodi ya Ushauri Jozani pamoja na watumishi wote kwa juhudi zao, ushirikiano na ushauri walionipatia jambo ambalo limeniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025.

Pia, nawapongeza kwa dhati viongozi wa jumuiya za wakulima na wafugaji, wakulima, wafugaji, watunza mazingira na wadau wote wa sekta za kilimo, maliasili na mifugo kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa ajili ya chakula na biashara pamoja na utunzaji wa misitu nchini.

81. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Viongozi Wateule wote wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, Masheha, Vikosi vya SMZ na SMT na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri wanayoendelea kuyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** na Waheshimiwa Wajumbe **nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.**


**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS**
**WAZIRI,**
**WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO,**
**ZANZIBAR**

## VIAMBATANISHO


**Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2022 - 2023, Zanzibar**

| Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga 2022 - 2023 - Zanzibar | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ZAO** | **2022** | | **2023** | |
| | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** |
| Muhogo | 34,501 | 202,520 | 37,549 | 220,412 |
| Mpunga wa juu | 26,243 | 23,683 | 25,591 | 29,993 |
| Mpunga wa Kumwagilia | 2,843 | 4,265 | 3,928 | 7,279 |
| Migomba | 6,086 | 52,337 | 8,664 | 96,976 |
| V/vikuu | 1,338 | 6,692 | 1,848 | 9,241 |
| Majimbi | 1,009 | 3,852 | 1,192 | 4,554 |
| J/kunde | 2,069 | 1,035 | 3,510 | 6,086 |
| V/Vidogo | 5,755 | 40,286 | 7,702 | 53,914 |
| Mtama | 609 | 231 | 744 | 283 |
| N/nyasa | 1,301 | 624 | 1,454 | 698 |
| Mahindi | 3,002 | 1,501 | 6,294 | 2,121 |
| Mbaazi | 663 | 2,142 | 851 | 2,748 |
| Uwele | 204 | 41 | 386 | 77 |
| Maboga | 592 | 2,807 | 1,420 | 6,731 |
| Chooko | 411 | 164 | | |
| Mboga na matunda | 17,692 | 66,304 | 21380 | 87971 |
| **Jumla** | **104,316** | **408,484** | **122,515** | **529,085** |


**Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2023**




**Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2023**



**Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2023**



**Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2023**



## Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2023 - Machi 2024

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2023/2024 | MAKADIRIO (JULAI - MACHI) | MAKUSANYO (JULAI-MACHI) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 45,561,000 | 33,661,000 | 44,572,500 | 132 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 1,500,000 | - | 167,500 | - |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 50,000,000 | 50,000,000 | 164,315,000 | 329 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 30,000,000 | 22,630,000 | 22,377,301 | 99 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 17,000,000 | 12,450,000 | 10,699,600 | 86 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 500,000 | 375,000 | 1,517,000 | 405 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI | 15,000,000 | 11,100,000 | 8,006,700 | 72 |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 548,000 | 500,000 | - | - |
| 1422068 | ADA YA MAZAO YA MIFUGO | 500,000 | 350,000 | 471,400 | 135 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 30,000,000 | 11,600,000 | 3,582,000 | 31 |
| | **JUMLA PEMBA** | **190,609,000** | **142,666,000** | **255,709,001** | **179** |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 315,100,000 | 242,600,000 | 236,222,653 | 97 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 25,000,000 | 5,400,000 | 4,161,000 | 77 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI | 1,217,300,000 | 1,028,800,000 | 950,514,048 | 92 |
| | **JUMLA** | **1,557,400,000** | **1,276,800,000** | **1,190,897,701** | **93** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | | | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 176,000,000 | 132,000,000 | 131,627,247 | 100 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 15,000,000 | 15,000,000 | - | - |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 10,000,000 | 7,000,000 | 3,818,800 | 55 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 65,000,000 | 63,500,000 | 3,834,000 | 6 |
| | **JUMLA** | **266,000,000** | **217,500,000** | **139,280,047** | **64** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | | | | |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 15,000,000 | 13,200,000 | 6,681,000 | 51 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 80,000,000 | 80,000,000 | - | - |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 30,000,000 | 22,500,000 | 19,273,000 | 86 |
| | **JUMLA** | **125,000,000** | **115,700,000** | **25,954,000** | **22** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | | | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 2,839,459,000 | 2,030,477,000 | 1,089,314,236 | 54 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 4,500,000 | 3,347,000 | 1,380,000 | 41 |
| | **JUMLA** | **2,843,959,000** | **2,033,824,000** | **1,090,694,236** | **54** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA** | | | | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 551,880,000 | **450,080,000** | **261,896,000** | 58 |
| | **JUMLA** | **551,880,000** | **450,080,000** | **261,896,000** | 58 |
| | **JUMLA UNGUJA** | **5,344,239,000** | **4,093,904,000** | **2,708,721,984** | **66** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **5,534,848,000** | **4,236,570,000** | **2,964,430,985** | **70** |

**Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2023 Hadi Machi, 2024**

| PROGRAM KUU/ PROGRAM NDOGO | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI, 2024 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MSHAHARA** | **MATUMIZI KAWAIDA** | **RUZUKU MSHAHARA** | **RUZUKU KAWAIDA** | **MAENDE LEO SMZ** | **MAENDELEO MUHISANI** | **JUMLA** |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **3,688,154,962** | **216,908,533** | **4,439,598,416** | **531,316,550** | **0** | **28,297,016,410** | **37,172,994,871** |
| SL010101: Kuendeleza miundombinu ya Umwagiliaji maji | 971,133,143 | 83,450,941 | | | | 21,300,000,000 | 22,354,584,084 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya kilimo - ZARI | | | 3,842,284,384 | 66,551,550 | | | 3,908,835,934 |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 2,717,021,819 | 133,457,592 | | | | 6,997,016,410 | 9,847,495,821 |
| SL010105: Karakana ya Matrekta | | | 597,314,032 | 464,765,000 | | | 1,062,079,032 |
| **PL0102: Maendeleo ya Raisilimali za Misitu** | **1,641,463,836** | **77,205,823** | **0** | **0** | **0** | **264,000,000** | **1,982,669,659** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 1,641,463,836 | 77,205,823 | | | | 264000000 | 1,982,669,659 |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **1,876,864,903** | **94,349,947** | **1,369,739,710** | **27,059,700** | **0** | **0** | **3,368,014,260** |
| SL010301 Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 1,876,864,903 | 94,349,947 | | | | | 1,971,214,850 |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - ZALIRI | | | 1,369,739,710 | 105,750,000 | | | 1,475,489,710 |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **4,350,435,476** | **740,913,816** | **0** | **0** | **0** | **0** | **5,091,349,292** |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 1,098,879,926 | 347,957,801 | | | | | 1,446,837,727 |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 234,948,811 | 62,956,015 | | | | | 297,904,826 |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 3,016,606,739 | 330,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3,346,606,739 |
| **JUMLA KUU** | **11,556,919,177** | **1,129,378,119** | **5,809,338,126** | **637,066,550** | **0** | **28,561,016,410** | **47,693,718,382** |

**Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2024/2025 |
|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 51,567,000 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 2,000,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 100,000,000 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 32,000,000 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 18,000,000 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 2,000,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | 15,000,000 |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 500,000 |
| 1422068 | ADAYA MAZAO YA MIFUGO | 550,000 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 35,000,000 |
| | **JUMLA PEMBA** | **256,617,000** |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 320,000,000 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 26,000,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | 1,400,000,000 |
| | **JUMLA** | **1,746,000,000** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 192,000,000 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 10,000,000 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 70,000,000 |
| | **JUMLA** | **272,000,000** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO NA MIFUGO** | | |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 15,000,000 |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 60,000,000 |
| | **JUMLA** | **75,000,000** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 2,757,450,000 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 45,000,000 |
| | **JUMLA** | **2,802,450,000** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 551,433,000 |
| | **JUMLA** | **551,433,000** |
| | **JUMLA UNGUJA** | **5,446,883,000** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **5,703,500,000** |

## Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025

| MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU KWA MWAKA 2023/2024, | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Program** | **Makadirio** | **Mshahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Ruzuku** | | **Maendeleo** | |
| | | | | **M/Mengineyo** | **Mshahara** | **SMZ** | **Muhisani** |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **101,485,914,448** | **6,371,463,844** | **1,612,200,000** | **1,676,500,000** | **9,520,100,000** | **27,500,000,000** | **54,805,650,604** |
| SL010101: Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji *(00000P001: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji)* | 26,198,340,456 | 1,658,340,456 | 540,000,000 | | | | 24,000,000,000 |
| *00000P034: Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji* | 1,500,000,000 | | | | | | 1,500,000,000 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya Kilimo na Mifugo-ZALRI | 9,035,300,000 | | | 1,200,400,000 | 7,834,900,000 | | |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 5,785,323,388 | 4,713,123,388 | 1,072,200,000 | | | | |
| *00000P028: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula* | 27,500,000,000 | | | | | 27,500,000,000 | |
| *00000P017: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)* | 203,099,000 | | | | | | 203,099,000 |
| *00000P035: Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha usalama wa Chakula (STREPHIT)* | 4,080,000,000 | | | | | | 4,080,000,000 |
| *00000P021: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (Agriconnect)* | 2,834,549,180 | | | | | | 2,834,549,180 |
| *00000P031: Mradi wa Kilimo Tija (USAID)* | 3,438,002,424 | | | | | | 3,438,002,424 |
| *00000P032: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula* | 18,750,000,000 | | | | | | 18,750,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SL010105: Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 2,161,300,000 | | | 476,100,000 | 1,685,200,000 | | |
| **PL0102: Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **4,503,918,212** | **2,791,118,212** | **530,000,000** | **0** | **0** | **0** | **1,182,800,000** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 3,321,118,212 | 2,791,118,212 | 530,000,000 | | | | |
| *00000P036: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)* | 500,000,000 | | | | | | 500,000,000 |
| *00000P037: Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR* | 682,800,000 | | | | | | 682,800,000 |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **13,890,428,864** | **3,229,928,864** | **660,500,000** | **0** | **0** | **2,500,000,000** | **7,500,000,000** |
| SL010301: Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 3,890,428,864 | 3,229,928,864 | 660,500,000 | | | | |
| *00000P029: Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo* | 2,500,000,000 | | | | | 2,500,000,000 | |
| *00000P033: Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP)* | 7,500,000,000 | | | | | | 7,500,000,000 |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 0 | | | 0 | 0 | | |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **8,227,289,080** | **6,741,189,080** | **1,486,100,000** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 2,578,134,108 | 1,829,134,108 | 749,000,000 | | | | |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 747,789,996 | 411,689,996 | 336,100,000 | | | | |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 4,901,364,976 | 4,500,364,976 | 401,000,000 | | | | |
| **JUMLA KUU** | **128,107,550,604** | **19,133,700,000** | **4,288,800,000** | **1,676,500,000** | **9,520,100,000** | **30,000,000,000** | **63,488,450,604** |

## Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mradi huu umeombewa TZS bilioni 31.701 ambapo TZS milioni 500.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 31.201 kutoka EXIM BANK ya Korea. Hadi kufikia Machi 2024 mradi umepata TZS bilioni **21.3** kutoka EXIM BANK ya Korea.

**Malengo kwa Mwaka 2023/2024**

i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 300 katika bonde la Cheju B, Uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima vya umwagiliaji maji pamoja na ujengaji wa misingi ya ndani kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani na Mlemele;

ii. Kusimamia maeneo yaliyojengwa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji yenye ukubwa wa hekta 1053 ikiwemo kuwapa mafunzo ya taaluma juu ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa kamati na wakulima viongozi sambamba na ukamilishaji wa utatuaji wa changamoto ya uvujaji maji katika bwawa la Chaani na ukamilishaji wa uungaji wa bomba za maji kwenye visima katika bonde la kilombero; na

iii. Kuwalipa fidia wananchi wataoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

**Utekelezaji wa Malengo**

i. Kazi za ujenzi na usimamizi wa mradi wa umwagiliaji maji katika bonde la Cheju A, Kilombero na Kinyasini zinaendelea. Aidha, ujenzi wa misingi ya kutolea maji ya ziada katika bonde la Cheju B imefikia kilomita 20 na ujenzi wa misingi ya ndani kwa kiwango cha saruji umefikia kilomita 30 ambapo sawa na asilimia 70.

ii. Kazi za usimamizi wa maeneo yaliyojengwa miundo mbinu mipya zinaendeleaKazi za Uungaji wa umeme wa njia kuu (3 phase line) katika skimu za umwagiliaji maji zinaendelea ambapo zimeanza katika bonde la Cheju na kufikiwa asilimia 80 kwa utekelezaji wake Cheju na kazi hii itaendelea kwa mabonde ya Kilombero na Kibokwa.

**Gharama za mradi:** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mradi huu unaombewa TZS bilioni 24.500 ambapo TZS milioni 500.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 24.000 kutoka EXIM BANK ya Korea.

**SHABAHA ZA 2024/2025**

i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagliaji yenye ukubwa wa eneo la hekta 131 katika bonde la Cheju B';

ii. Ujenzi wa mitaro midogo yenye urefu wa Kilomita 20 kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Kilombero, Cheju na Kinyasini;

iii. Ununuzi wa mitambo midogo ya kusaidia kazi za kilimo, palizi na uvunaji katika mobende ya umwagiliaji; na

iv. Kusimamia maeneo yalitojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji

## Kiambatanisho Nam 7B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2023/2024** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS bilioni 22.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufikia Marchi 2024 Mradi huu haujaweza kutumia kutokana na kuchelewa kukamilisha taratibu za manunuzi. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kukarabati maghala na ununuzi wa chakula |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:** Kuhakikisha haki ya upatikanaji wa chakula katika ngazi ya kaya na taifa inafikiwa. |
| **Malengo ya mwaka 2023/2024**<br>i. Kukarabati ghala moja la kuhifadhia chakula; na<br>ii. Kununua na kuijengea mitambo ya baridi katika maghala. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2023/2024**<br>i. Kutafuta washauri elekezi kwa ajili ya kazi ya ukarabati wa Maghala ya kuhifadhia chakula<br>ii. Kutafuta Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ukarabati wa Ghala la Malindi Unguja |
| **Kwa mwaka 2024/2025:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 27.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| **Kazi zilizopangwa 2024/2025**<br>i. Kumalizia ukarabati wa maghala<br>ii. Kununua na kujenga mitambo ya baridi<br>iii. Kununua chakula cha akiba |

## Kiambatanisho Nam. 7C: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)

**Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi uliombewa jumla ya TZS milioni 485.558 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 Mradi umepokea jumla ya TZS milioni **159.589** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**Malengo ya Mwaka 2023/2024**

i. Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu;
ii. Kuendelea na malipo ya wakandarasi wa ujenzi wa ghala la Pemba;
iii. Kuendelea na shughuli za kutoa elimu ya sumukuvu kwa wadau kwa mfano wakulima;
iv. Kushiriki katika maonesho ya kitaifa;
v. Kutengeneza vifaa vya uelimishaji wa jamii k.v vipeperushi mabango kofia na fulana;
vi. Kununua vifaa kwa ajili ya maghala Unguja na Pemba;
vii. Usimamizi na uendeshaji wa ofisi; na
viii. Kwa kushirikiana na VETA na Mamalaka ya Ufundi Stadi Zanzibar VTA mradi utaendelea kuwapa mafunzo ya utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa vijana 40 Unguja na Pemba

**Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2023/2024**

i. Ujenzi wa Ghala la Dodeani Pemba umefikia asilimia.
ii. Jumla ya wananchi 175 wamepatiwa mafunzo ya Sumu Kuvu
iii. Jumla ya vijana 40 wamepatiwa mafunzo ya utengenezaji wa vizimba Unguja na Pemba

**Kwa mwaka 2024/2025:** Mradi unaombewa jumla ya TZS milioni 203.099 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Malengo kwa mwaka 2024/2025**

i. Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu;
ii. Kuendelea na shughuli za kutoa elimu ya sumukuvu kwa wadau kwa mfano wakulima;
iii. Kushiriki katika maonesho ya kitaifa;
iv. Kutengeneza vifaa vya uelimishaji wa jamii k.v vipeperushi mabango kofia na fulana;
v. Kununua vifaa kwa ajili ya maghala Unguja na Pemba;
vi. Usimamizi na uendeshaji wa ofisi;

## Kiambatanisho Nam. 7D: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni 18.750 chini ya udhamini wa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**Malengo ya Mradi:**

i. Kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi; na

ii. Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula.

**Maeneo Makuu ya Mradi:**

i. Kuongeza utoaji wa huduma za utafiti, mbegu na ugani

ii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde manane (8)

iii. Kufanya uratibu wa Mradi

**Shabaha kwa mwaka 2024/2025**

i. Kufanya ukarabati wa majengo wa maabara za ZARI za Kizimbani na Matangatuani;

ii. Kuendeleza tafiti za mazao ya mpunga, muhogo, ndizi na tungule;

iii. Kufanya utafiti wa afya ya udongo;

iv. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu yaliyopo Bambi, Kibondemzungu, Mwera, Kizimbani na Ole;

v. Kufanya ukarabati wa vituo vinne vya huduma za wakulima katika mashamba ya Bumbwisudi (2), Mtwango (1) na Kibokwa (1);

vi. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;

vii. Kufundisha wakulima njia bora za kilimo kwa kutumia teknolojia, kilimo biashara na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya mavuno;

viii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji hekari 434 katika mabonde 8 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Weni, Saninga na Kinyakuzi. Ukarabati utahusisha njia za kupitishia maji, kuchimba visima, njia za ndani nakadhalika;

ix. Kununua vifaa kwa ajili ya kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani, vifaa hivyo ni, trekta ndogondogo za kulimia, kupandia, kupalilia na kuvunia.

## Kiambatanisho Nam. 7E: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT)

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 8.563 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Umoja wa Nchi za Ulaya. Hadi kufika Machi 2024 Mradi umepata jumla ya TZS bilioni 4.698 kutoka kwa washirika wa Maendeleo. |
| **Malengo ya mwaka 2023/2024**<br>i. Kuwajengea uwezo wakulima 10,500, hasa wanawake kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora ambavyo vinazingatia mfumo wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi;<br>ii. Kuongeza thamani kwa kujenga majengo mawili ya kusindika mazao, kushughulikia masoko na kilimo biashara;<br>iii. Kuwajengea uwezo wanawake;<br>iv. Kuongeza kipato cha wakulima wadogo 1,767 kwa kuwasogezea huduma za fedha kuendeleza uzalishaji wa mazao ya mboga, viungo na matunda;<br>v. Kuwapatia mitaji wajasiriamali na wakulima wadogo vikundi 45 kuendeleza miradi ya kilimo cha horticulture pamoja na usindikaji;<br>vi. Kujengea uwezo wakulima kwa utaalamu wa Viwango endelevu vya Hiari (VSS) pamoja na mchakato wa kuwa na vyeti vya uthibitisho wa mazao;<br>vii. Kufanya Utafiti wa kudhibiti viumbe waharibifu wa mazao, pamoja na kuchunguza mabaki ya madawa ya mimea katika mazao; na<br>viii. Kuendeleza mpango wa kusambaza taarifa za masoko na elimu kwa wadau. |
| **Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2023/2024**<br>i. Kufanya tathmini ya mahitaji ya mazao ya mboga na matunda katika mahoteli ya Zanzibar<br>ii. Kutoa ruzuku kwa wakulima wanaolima mazao ya mboga na matunda kwa Unguja na Pemba<br>iii. Kujenga kituo cha kuhifadhia mazao Wilaya ya Chake Chake Pemba |
| **Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi umepangiwa kiasi cha TZS bilioni **2.834** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Umoja wa Nchi za Ulaya |
| i. Kuendelea kuwajengea uwezo wakulima 10,500, hasa wanawake kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora ambavyo vinazingatia mfumo wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi;<br>ii. Kuongeza thamani kwa kujenga majengo mawili ya kusindika mazao, kushughulikia masoko na kilimo biashara;<br>iii. Kuongeza kipato cha wakulima wadogo 1,767 kwa kuwasogezea huduma za fedha kuendeleza uzalishaji wa mazao ya mboga, viungo na matunda;<br>iv. Kuwapatia mitaji wajasiriamali na wakulima wadogo vikundi 45 kuendeleza miradi ya kilimo cha horticulture pamoja na usindikaji;<br>v. Kujengea uwezo wakulima kwa utaalamu wa Viwango endelevu vya Hiari (VSS) pamoja na mchakato wa kuwa na vyeti vya uthibitisho wa mazao;<br>vi. Kufanya Utafiti wa kudhibiti viumbe waharibifu wa mazao, pamoja na kuchunguza mabaki ya madawa ya mimea katika mazao; na<br>vii. Kuendeleza mpango wa kusambaza taarifa za masoko na elimu kwa wadau wa mazao ya bustani. |

## Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kilimo Tija

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2023/2024** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni **2.340** kutoka kwa Washirika wa Maendleo – USAID. Hadi kufikia Machi 2024 Mradi umepata jumla ya TZS bilioni **2.006** Kutoka kwa washirika wa Maendeleo |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuendeleza fursa za kiuchumi katika mifumo ya masoko ya mazao ya mboga na matunda, hasa kwa vijana.<br><br>**Malengo Makhsusi ya Mradi**<br>i. Kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao ya mboga na matunda kwa kuongeza fusra za ajira na ujasiriamali;<br>ii. Kuongeza upatikanaji wa teknpolojia za kilimo zinazoimarisha uzalishaji wa kilimo kibiashara na unaozingatia mabadiliko ya tabianchi; na<br>iii. Kuimarisha mazingira wezeshi ya kuendeleza mifumo ya masoko. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2023/2024**<br>i. Kusaidia shughuli za ugani katika Wizara ya Kilimo ili kuweza kufikisha huduma bora za ugani kwa wakulima kwa kuimarisha uwezo wa mabwana shamba pamoja na kushajiisha wadau zaidi wa ugani;<br>ii. Kuhimiza upatikanaji na matumizi ya teknolojia za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi na kuongeza tija ili kuhakikisha kuwepo kwa uzalishaji wa mazao mwaka mzima huku ikisaidia wakulima kufikia masoko;<br>iii. Kuongeza jitihada katika kuimarisha mabaraza ya vijana katika ngazi ya wilaya ili kuwajenga uwezo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuendeleza biashara katika minyororo ya thamani;<br>iv. Kusaidia jitihada za sekta binafsi katika kuwawezesha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kufikia mitaji itakayosaidia biashara zao;<br>v. Kuisaidia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI kuandaa benki ya hifadhi ya mimea mazao kwa mazao ya mboga na matunda yenye asili ya Afrika;<br>vi. Kushirikiana na sekta binafsi katika kusaidia kuandaa ramani ya udongo ya Zanzibar;<br>vii. Kusaidia kuimarisha vikundi vya ushirika vya mboga na matunda Zanzibar katika maeneo ya uzalishaji, utawala bora na upatikanaji wa mitaji; na<br>viii. Kusaidia maandalizi ya mafunzo endelevu ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2023/2024**<br>i. Jumla ya mabwana 99 wamepatiwa mafunzo ya ugani;<br>ii. Jumla ya vijana 134 wamepatiwa mafunzo ya kilimo tija; na<br>iii. Kushiriki katika maonesho ya nane nane na siku ya chakula duniani. |
| **Kwa mwaka wa fedha 2024/2025** Mradi huu umepanga kutumia TZS bilioni 3.438 kutoka washirika wa Maendeleo |
| **Malengo kwa mwaka 2024/2025:** Kuendelea kukamilisha malengo ya 2023/2024. |

## Kiambatanisho Nam. 7G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)

| |
|---|
| **Kwa mwaka wa fedha 2023/2024,** mradi ulitengewa kiasi cha TZS milioni 514.000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Umoja wa Ulaya. Hadi kufikia Machi 2024 Mradi umeingiziwa TZS milioni **264** sawa na asilimia **51.36** |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:** Kuiwezesha asali bora inayozalishwa kwa njia endelevu ya mazingira kupenya katika masoko. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2023/2024**<br>i. Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki;<br>ii. Uanzishwaji na uendelezaji wa mashamba darasa ya wafugaji nyuki (manzuki), na<br>iii. Kuwaunganisha wazalishaji wa mazao ya nyuki na masoko |
| **Utekelezaji 2023/2024**<br>i. Jumla ya wafugaji nyuki 724 kutoka vikundi 96 wamepatiwa mafunzo<br>ii. Jumla ya mashamba darasa 3 (apiaries) yameanzishwa katika mikoa ya Wete na Mkoani<br>iii. Utafiti wa kujua aina za asali zinazozalishwa unaendelea<br>iv. Kuwapatia mafunzo ya ujengaji wa Mizinga mafunzi seremala 20 kutoka kwa wakufunzi wa Chuo cha nyuki Tabora. |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mradi umetengewa kiasi cha TZS milioni 500.000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Umoja wa Ulaya. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa**<br>i. Kuendelea na tafiti za nyuki<br>v. Kutoa mafunzo ya nyuki |

### Kiambatanisho Nam. 7H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2023/2024** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS Bilioni 2.000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufika Machi 2024 Mradi haukuingiziwa fedha |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mazingira ya chinjio na karantini, kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za madume wa ng'ombe. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi**<br>1. Kuimarisha miundo mbinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2023/2024**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen; na<br>ii. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba.<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi. |
| **Kazi zilizotekelezwa:** Hakuna |
| **Kwa mwaka 2024/2025** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni 2.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2024/2025**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen; na<br>ii. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba.<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi. |

## Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha usalama wa chakula STREPHIT)

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni **4.080**. |
| **Malengo kwa Mwaka 2024/2025** |
| i. Kuongeza upatikanaji mazao ya Kilimo yaliyosalama na bora kwa masoko ya Kitaifa na Kimataifa;<br>ii. Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa udhibiti rasmi wa uingizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo; na<br>iii. Huduma za Kitaifa za Afya ya Mimea kutumia ufuatiliaji unaoaminika na mifumo ya ulinzi wa mimea. |
| **Shabaha za Mradi:**<br><br>i. Kufanyika kwa warsha ya siku mbili ambayo imezungumzia masuala mazima ya uandaaji wa mtaala mpya kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaojishughulisha na utoaji wa huduma za afya ya mimea nchini amapo washiriki waligusia maeneo yote muhimu yanayogusa tasnia nzima ya huduma za afya ya mimea;<br><br>ii. Kuanzisha kwa mfumo wa utoaji wa cheti cha usafi wa mimea kwa njia ya mtandao (ATMIS) ambapo malipo ya yatakuwa chini ya mfumo wa Zanmalipo;<br><br>iii. Uandaaji wa Kitabu cha agizo la uingizaji wa bidhaa ndani ya mfumo wa utoaji cheti cha usafi wa mimea kwa njia ya mtandao (IMPORT ORDER BOOK-ATMIS);<br><br>iv. Kununua Kombo Tool Box kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa utoaji wa taarifa za wadudu, maradhi ya mimea na mazao yanayoingia na kutoka nchini;<br><br>v. Kushajihisha Mpango wa utafiti utakaoeleza uundaji wa orodha ya wadudu nchini;<br><br>vi. Kukarabatiwa kwa maabara na za wadudu Unguja na Pemba na kujengewa uwezo kwa wataalamu watakaoendesha shughuli za maabara hizo;<br><br>vii. Kusaidia katika utayarishaji wa Sheria na Kanuni za Zanzibar; na<br><br>viii. Kusaidia utayarishaji upya wa muundo wa URT-NPPO katika Shirika la Kimataifa la masuala ya Ulinzi wa mimea (IPPC). |

## Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS milioni 682.800 kutoka Global Environmental Facility **(GEF)** |
| **Malengo kwa Mwaka 2024/2025** |
| i. Uhifadhi wa Misitu katika maeneo ya Kaskazini A na B<br>ii. Kushirikisha sekta za Kilimo, Mazingira, Ardhi na sekta nyengine zenye mnanasaba na Uhifadhi wa Misitu katika kuhifadhi na kusimamia rasilimali hiyo. |
| **Shabaha za Mradi:**<br>i. Kukarabati majengo<br>ii. Kuhamasisha jamii zinazozunguka Wilaya za Kaskazini A na B<br>iii. Kutoa elimu ya Uhifadhi. |

## Kiambatanisho Nam. 7K: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa kuwa TZS bilioni 1.5 chini ya Ufadhili wa Serikali ya Korea |
| **Malengo ya Mradi**<br>i. Kuchangia uimarishaji wa uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato cha wakulima wa mpunga Zanzibar<br>ii. Kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji |
| **Shabaha kwa mwaka 2024/2025**<br>i. Kununua matrekta ya kilimo katika mabonde ya mradi wa Umwagiliaji kwa ajili ya jumuiya za wakulima kwa kuimarisha zao la mpunga;<br>ii. Kununua matrekta, na machine ya kuvunia mpunga kwa ajili ya Taasisi ya Huduma za zana za kilimo kwa kutolea mafunzo kwa jumuiya za wakulima wa mpunga;<br>iii. Kuboresha miundombinu ya kilimo kwa kutengeneza njia za mashambani, vivukio vya matrekta pamoja na maeneo ya kuanikia mpunga;<br>iv. Kujenga maeneo ya kuhifadhia mazao ya mfunga, matrekta, pamoja na uchimbaji wa kisima katika kuongeza upatikanaji wa maji mengi bonde la Chaani<br>v. Kununua vifaa vya usimamizi na ufuatiliaji wa vyanzovya maji katika maeneo ya umwagiliaji maji. |

**Kiambatanisho Nam. 7L: Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi**

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni 7.500 Mkopo kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo IFAD na OPEC. |
| **Malengo ya Mradi**<br>i. Kuchangia katika kuleta mageuzi kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya kukuza hali hali ya mazisha kwa jamii, kuongeza uhakika wa chakula na vilevile kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa; na<br>ii. Kukuza kipato, uhimilivu wa tabia nchi, kuongeza lishe kwa wazalishaji wadogowadogo wa maziwa na ushiriki wao kikamilifu na bora katika mnyonyoro wa thamani wa maziwa. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi**<br>i. Mpango wa uzalishaji wa maziwa wenye tija na himilivu;<br>ii. Ushirikishwaji katika minyonyoro bora ya thamani, uwekezaji binafsi, unywaji wa maziwa na pamoja na sera. |
| **Shabaha kwa mwaka 2024/2025**<br>i. Uanzishaji wa vituo vidogo vya ukusanyaji wa maziwa katika maeneo maalum;<br>ii. Ukarabati wa vituo vya ukusanyaji na usarifu wa maziwana (MCCs) viliopo na ujenzi wa vituo vingine vipya;<br>iii. Ununuzi wa mitamba bora ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa;<br>iv. Ujenzi wa viwanda vidogo vya kusarifu maziwa;<br>v. Ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu yaliyopo Kizimbani;<br>vi. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia bora za kisasa;<br>vii. Kufundisha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa njia bora za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuzingatia njia bora za uhimilivu wa tabia nchi; na<br>viii. Kuendeleza ujenzi wa mitambo ya biogas Unguja na Pemba kwa lengo la upatikanaji wa nishati ya kupikia na mbolea bora kwa ajili ya uzalishaji wa mazao pamoja na malisho ya mifugo. |

**Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2024/2025**

